PUB 195US (9-23) Swahili

# Matakwa ya Utambulisho na Makazi Kwa Raia wa Marekani

Kama sehemu ya jitihada ya taifa zima ya kuboresha utoaji wa hati salama za utambulisho, jimbo la Pennsylvania linahitaji hati zifuatazo kutoka kwa Raia wa Marekani wanaotuma ombi la Leseni ya Dereva, Kibali cha Mwanafunzi au Kitambulisho (ID) au Raia wa Marekani wanaohamisha Leseni ya Dereva au Kitambulisho nje ya jimbo.

**TAFADHALI KUMBUKA: Ikiwa unatuma ombi la bidhaa ya REAL ID tafadhali rejelea Orodha ya Ukaguzi wa Hati ya REAL ID iliyo kwenye tovuti ya PennDOT' katika https://www.dmv.pa.gov/REALID kwa maelezo zaidi.**

## Matakwa ya Umri kwa Raia wa Marekani

Watu binafsi wanaotuma ombi la Leseni ya Dereva Isiyo ya Biashara lazima wawe na umri usiopungua miaka 16.

Watu binafsi wanaotuma ombi la Kitambulisho (ID) lazima wawe na umri usiopungua miaka 10.

Watu binafsi wanaohamisha Leseni ya Dereva Isiyo ya Biashara lazima wawe na umri usiopungua miaka 16 1/2.

Watu binafsi wanaotuma ombi la Kibali cha Mwanafunzi cha Pennsylvania lazima wawe na umri usiopungua miaka 16.

Vibali vya Wanafunzi wa nje ya jimbo haviwezi kuhamishwa hadi Pennsylvania.

Watu binafsi wanaotuma ombi la au wanaohamisha Leseni ya Dereva ya Biashara lazima wawe na umri usiopungua miaka 18 kwa uendeshaji gari ndani ya mipaka ya jimbo au miaka 21 au zaidi kwa uendeshaji gari baina ya majimbo.

## Wakazi wa Pennsylvania

Ikiwa una umri wa miaka 18 na mkazi wa Pennsylvania utahitajika kuonyesha:

- ☐ fomu moja ya utambulisho kutoka Orodha ya A, na
- ☐ Kadi yako ya Ruzuku ya Serikali.

Ikiwa una umri wa miaka 18 au zaidi na mkazi wa Pennsylvania utahitajika kuonyesha:

- ☐ fomu moja ya utambulisho kutoka Orodha ya A,
- ☐ fomu mbili za thibitisho la makazi kutoka kwenye Orodha ya B, na
- ☐ Kadi yako ya Ruzuku ya Serikali.

## Wakazi Wapya wa Pennsylvania

Wakazi wapya wa Pennsylvania walio na leseni halali ya dereva kutoka kwenye jimbo jingine nchini Marekani lazima wapate Leseni ya Dereva ya Pennsylvania ndani ya siku 60 baada ya kuhamia PA na kusalimisha leseni ya dereva na/au kitambulisho cha nje ya jimbo.

Ikiwa wewe ni mkazi mpya wa Pennsylvania na leseni yako ya dereva ya jimbo la awali imeisha muda wa kutumika kwa zaidi ya miezi sita au huna leseni ya dereva ya jimbo lako la awali, utahitajika kutuma ombi la Kibali cha Mwanafunzi cha PA na kufanya Mitihani ya Macho, Maarifa na Barabara.

Wakazi wapya wa Pennsylvania walio na leseni halali ya dereva kutoka himaya au miliki ya Puerto Rico au Marekani wanaweza kuhamisha leseni yao halali ya dereva hadi Leseni ya Dereve Isiyo ya Biashara ya PA.

Wakazi wapya wa Pennsylvania walio na leseni halali ya dereva ya biashara (CDL) kutoka kwenye jimbo jingine Marekani wanaweza kuhamisha CDL yao hadi PA CDL.

Ikiwa una umri wa miaka 18 na mkazi mpya wa Pennsylvania utahitajika kuonyesha:

- ☐ fomu moja ya utambulisho kutoka Orodha ya A,
- ☐ Kadi yako ya Ruzuku ya Serikali, na
- ☐ leseni yako ya dereva na/au kitambulisho cha nje ya jimbo.

Ikiwa una umri wa miaka 18 au zaidi na mkazi mpya wa Pennsylvania utahitajika kuonyesha:

- ☐ fomu moja ya utambulisho kutoka Orodha ya A,
- ☐ fomu mbili za thibitisho la makazi kutoka kwenye Orodha ya B,
- ☐ Kadi yako ya Ruzuku ya Serikali, na
- ☐ leseni yako ya dereva na/au kitambulisho cha nje ya jimbo.

## ORODHA YA A:

**Fomu za Utambulisho Zinazokubalika kwa Raia wa Marekani:**

- ☐ Cheti cha Kuzaliwa chenye muhuri uliotunishwa *(kilichotolewa Marekani na shirika la serikali lililoidhinishwa, ikiwa ni pamoja na*
  *himaya za Marekani au Puerto Rico. Vyeti vya Kuzaliwa Visivyo vya Marekani havitakubaliwa.)*
  ***Kumbuka:*** *Vyeti vya Kuzaliwa kutoka Puerto Rico lazima viwe na tarehe ya kutolewa ya 7/1/10 au baadaye ili vikubaliwe.*
    - *Ikiwa cheti chako cha kuzaliwa kinajumuisha lugha inayosema kuwa rekodi ya kuzaliwa si ushahidi wa uraia wa Marekani, huenda ukahitajika kutoa hati zaidi.*
- ☐ Cheti cha Uraia wa Marekani (USCIS Fomu N-560 au N-561)
- ☐ Ripoti ya Balozi ya Kuzaliwa Ng`ambo (DOS Fomu FS-240)
- ☐ Cheti cha Kuandikisha Uraia (USCIS Fomu N-550 au N-570)
- ☐ Pasipoti Halali ya Marekani

***KUMBUKA: Ni Pasipoti halali na hati asili tu zitakazokubaliwa. Ikiwa jina lililo kwenye hati yako asili linatofautiana na jina lako la sasa, lazima utoe hati inayohusisha majina, kama vile Cheti cha Ndoa asili, Amri ya Talaka, au hati ya Agizo la Mahakama.***

## ORODHA YA B:

**Orodha Inayokubalika ya Hati za Thibitisho la Makazi kwa Waombaji wa Miaka 18 au Zaidi: Thibitisho la hati za makazi lazima liwe na jina lako na anwani rasmi ya barabara ya Pennsylvania.**

- Barua iliyo na muhuri wa posta/lebo za kifurushi kupitia USPS, UPS, FedEx nk.
- Fomu/hati ya malipo ya A W-2
- Mikataba ya kupangisha au hati za mkopo wa nyumba
- Rekodi Rasmi za Kodi zinazoonyesha jina na anwani ya sasa
- Leseni ya dereva au kitambulisho cha picha ya sasa ambayo inatumika ya PA
- Kadi ya usajili wa gari ya PA
- Kadi ya bima ya gari
- Bili ya huduma za msingi iliyozalishwa na kompyuta ikionyesha jina na anwani yako (rununu, kebo, umeme, gesi)

***KUMBUKA:*** *Ikiwa unaishi na mtu na huna bili kwa jina lako, bado utahitajika kutoa mathibitisho mawili ya makazi. Thibitisho moja ni la kuleta Leseni ya Dereva au Kitambulisho cha mtu unayeishi naye kwenye Kituo cha Leseni za Dereva. Pia utahitaji kutoa thibitisho la pili la makazi kama vile barua iliyo na muhuri wa posta/lebo za kifurushi kupitia USPS, UPS, FedEx nk. lililo na jina na anwani yako. Lazima anwani ilingane na ile ya mtu unayeishi naye.*

## TAFADHALI KUMBUKA

Lazima hati zote zionyeshe jina na tarehe ya kuzaliwa ileile, au uhusiano baina ya taarifa zilizo kwenye hati. Hati za ziada zinaweza kuhitajika ikiwa uhusiano baina ya hati hauwezi kutambiliwa (mfano, Cheti cha Ndoa, Agizo la Mahakama la mabadiliko ya jina, Amri ya Talaka, n.k.)